(1) Jina langu ni Walugembe John. Mimi ni mwanafunzi katika shule ya sekondari ya Wazalendo na niko katika kidato cha kwanza. Mama yangu ni Bi. Maria Mwema na ni mtu mzuri sana kwa sababu jirani yetu husema hivyo. Baba yangu anaitwa Bw. Mrefu na ni mwanamume mpole sana. Familia yetu ina watoto wawili, mimi na dada yangu Izaura. Mimi ni kifungua mimba na Izaura ni kitinda mimba. Wazazi wetu ni wazazi wazuri kwa sababu huwa wanatupatia kila kitu ambacho tunahitaji kwa mfano kutulipia karo shuleni, kutununulia vyakula na vinywaji na hata kuhaikisha kwamba chakula kipo nyumbani. Mama yetu ni mwanabiashara na ana duka la kuuza bidhaa. bidhaa ambazo huuza ni kama mkate, majani, sukari, chumvi, sabuni, mchele na mengine. Duka la mama yangu liko karibu na kanisa la walokole ambao huomba kila Jumamosi na Jumapili. Pia karibu na duka la mama kuna kituo cha polisi ambapo wahalifu hupelekwa,

Baba yetu ni mkulima maarufu ambaye hupanda mimea na matunda pia kufuga Wanyama na ndege. Mimea ambazo anapanda ni kama mahindi maharagwe, njugu, kahawa, migomba. mihogo na matunda kama tikitimaji, chungwa, chenza,maembe, fenesi, ndimu, papai. mzabibu na tomoko. Wanyama ambao anawafuga ni kama ngomba, mbuzi, kondoo, kuku na bata.

Hao Wanyama wakiwa wengi yeye huuza kila kuku shilingi elfu ishirini na tano, kila ngombe milioni moja na nusu na kila mbuzi shilingi elfu mia moja na themanini. Mazao kama mchele, maharagwe na ndizi pia anapeleka sokoni kuyauza. Mimi ninapenda familia yangu kwa sababu huwa tunaishi kwa Amani, upendo na umoja.

MASWALI

1, Jina la msemaji ni nani?……………………………………………………………………………………………………………

2, Anasomea katika shule gani?………………………………………………………………………………………………………

3, Mama yake ni nani?.........................................................................................................................

4, Baba yao ni nani?............................................................................................................................

5, Katika duka la mama Walugembe John anauza bidhaa gani?.........................................................................................................................................
.........................................................................................................................................................

6, Duka la mama yake liko karibu na nini?.........................................................................................

7, Baba yao anafanya nini?...................................................................................................................

8, Taja matunda ambazo zimetajwa katika hadithi hii………………………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………………………………………

9, Taja Wanyama ambao wametajwa katika hadithi hii…………………………………………………………………………….

10, Taja mazao ambazo baba yao hupeleka sokoni kuuza………………………………………………………………………………………………………………………………………………

(2) Ulifia shuleni asubuhi kama umechelewa na mwalimu wako akakuita ofisini akitaka kujua ni kwa nini.

Andika dayalojia kati YAKO na MWALIMU wako.

3, SOMS SHAIRI IFUATAYO KISHA UJIBU MASWALI

Shikeni jembe limeni. kila mumea pandeni
Sote kazi shirikeni, mazao tele vuneni

Mboga uzeni sokoni, nafaka pia matunda,
Shime tushikilieni, uchumi wake Uganda

Kula siyo mashindano, kidogo na chenye lishe,
Siyo tu vile vinono, kila aina itoshe,

Cha kuliwa hadharani, sifiche ukale mbali,
Mi nikiwa hotelini, nala nanywa kiasili,

Vyanzo vya maji ni vyetu, tusiuwe kwa kulima
vinamasi na misitu, tusikate na kuchoma

vichupa na karatasi, marufu kama kavera,
Si tupe kama chapasi, rutuba itaparara

MASWALI

1, Shairi hili lina beti ngapi?..........................................................................................

2, Shairi hili lina mistari mingapi?.................................................................................

3, Unapata ujumbe gani kutoka shairi hili………………………………………………………………………….

4, Ipe hili shairi kichwa……………………………………………………………………………………………………

5 kibwagizo cha ubeti wa kwanza ni nini?.......................................................................

6, Shairi hili lina pande ngapi……………………………………………………………………………………….

SARUFI

Andika sentensi zifuatazo katika wakati ujao TA

1 Mama anapika chakula ………………………………………………………………………………………………

2, Mtoto amecheza mpira ………………………………………………………………………………………………

3, Mwalimu anafundisha …………………………………………………………………………………………….

4, Ninaandika kazi ………………………………………………………………………………………………

5, Leo nimepata pesa ……………………………………………………………………………………………….

6, Mtoto anakunywa chai ……………………………………………………………………………………………….

7, Mama analala ……………………………………………………………………………………………….

8, Mwimbaji aliimba wimbo ………………………………………………………………………………………………

9, Shangazi anapika mchele ……………………………………………………………………………………………….

10, Kaka anakamua ngombe ……………………………………………………………………………………………….

**MWISHO**